

TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA



TAARIFA KWA UMMA

KUFUNGWA RASMI KWA ZOEZI LA UDAHILI KWA WAOMBAJI WA SHAHADA YA KWANZA KWA MWAKA 2016/17

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) inautangazia Umma kuwa zoezi la kupokea maombi ya kujiunga na masomo ya elimu ya juu kwa mwaka wa masomo 2016/2017 limefungwa rasmi. Orodha ya majina ya waliochaguliwa ilishatangazwa na vyuo husika. Wote waliochaguliwa wanaweza kuona vyuo na programu walizochaguliwa kupitia tovuti ya tume www.tcu.go.tz ([view provisional results for 2016/17](#)).

Hivyo Tume inapenda kuwatangazia wote waliodahiliwa na Umma kwa ujumla kwamba:

- Mfumo wa pamoja wa udahili (CAS) kwa mwaka wa masomo 2016/17 sasa umefungwa rasmi.
- Waombaji wote waliopangiwa vyuo wanatakiwa wawe wamesharipoti kwenye vyuo husika kwa usajili na taratibu nyingine kabla ya muda wa usajili kuisha
- Taratibu zote za kuhama chuo au programu zitafanyika vyuoni na kuthibitishwa na Tume. Mwisho wa kupokea maombi ya uhamisho ni tarehe **18 Novemba, 2016** na hakuna maombi yatakayopokelewa baada ya muda huo kuisha.

Imetolewa na
Katibu Mtendaji

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania
15/11/2016